

## Maelekezo ya Barua kutoka kwa Shirika

Ili kutuma ombi la UNM Care au Out-of-County Care, lazima utupatie hati zinazothibitisha utambulisho wako na mahali unakoishi.

Wakati mwingine watu huwa hawana hati hizi. Ikiwa huna, unaweza kumwomba mhudumu anayeshughulikia suala lako, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na linalojua hali yako litoe taarifa iliyoandikwa inayothibitisha utambulisho wako na/au mahali unakoishi. Hii inaitwa barua ya uthibitisho. Uthibitisho unamaanisha kuthibitisha au kukiri kwamba jambo fulani ni kweli.

Unaweza kumpatia mmoja wa watu hawa maelekezo yaliyo hapa chini.

Mpendwa Mwandishi wa Barua,

Asante kwa kuniandikia barua. Hapa kuna baadhi ya maelekezo.

- **Unaweza kutumia Barua ya Uthibitisho wa Shirika ya mfano** iliyo katika ukurasa unaofuata. Nakili barua hiyo ya mfano na uibandike kwenye ukurasa ulio na lebo ya shirika lako (ikiwa unayo), ujaze nafasi tupu, ufute sentensi zozote zisizotumika na utie sahihi.
- **Kuandika Barua ya Uthibitisho wa Shirika kwa mkono.** Tumia barua ya mfano kama mwongozo kuandika barua yako mwenyewe. Jumuisha tu taarifa zinazohusiana na kile unachothibitisha (utambulisho wa mgonjwa na/au mahali anakoishi). Kwa barua zilizoandikwa kwa mkono au barua zisizo na lebo, tafadhali jumuisha kadi rasmi ya maelezo ya mawasiliano ya biashara au hati kama hiyo.
- Barua zote lazima ziwe na tarehe, jina la mwandishi, cheo, nambari ya simu na barua pepe ya mawasiliano na sahihi.
- Barua zinaweza kupeanwa kwa mgonjwa moja kwa moja ili aziwasilishe mwenyewe au zinaweza kutumwa kwa barua ya posta kwa UNM Financial Assistance katika 1131 University Blvd, Suite D, Albuquerque, NM 87102 au zinaweza kutumwa kwa barua pepe kwa [financialassistance@salud.unm.edu](mailto:financialassistance@salud.unm.edu) au kwa anwani ya barua pepe ya mwakilishi wa mgonjwa.
- Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali pigia simu kitengo cha Usaidizi wa Kifedha cha UNM kwa 505 272-2521.

## Barua ya Uthibitisho wa Shirika ya Mfano

Tarehe: \_\_\_\_\_

Ninaandika ili kukupatia taarifa kuhusu \_\_\_\_\_  
jina la mgonjwa

Shirika hili, \_\_\_\_\_, limekuwa likishirikiana na  
jina la shirika

\_\_\_\_\_ tangu \_\_\_\_\_  
jina la mgonjwa mwezi/mwaka

Kulingana na ninavyomjua mtu aliyeorodheshwa hapa chini, ninaweza kusema kuwa:

\_\_\_\_\_ ni jina sahihi.

Mgonjwa huyu anaishi \_\_\_\_\_.

Tafadhali kubali taarifa hii kama hati ya ombi lake la UNM Care au Out of County Care.

\_\_\_\_\_  
Sahihi

\_\_\_\_\_  
Jina

\_\_\_\_\_  
Cheo

\_\_\_\_\_  
Nambari ya simu na/au anwani ya barua pepe